# OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA / UJIJI

**SHULE YA SEKONDARI MWANANCHI**
**S.L.P 53,**
**KIGOMA.**

**18/12/2020**

Kumb. Na: MWCHSS/B.33/22

JINA LA MWANAFUNZI: ..........................................................................
SHULE YA MSINGI: ................................................
S.L.P ......................
KIGOMA.

### YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWANANCHI</u>

**1.0. UTANGULIZI**

Nafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule hii. Shule ya Sekondari Mwananchi ipo kata ya Mwanga Kusini, karibu na maungio ya barabara kuu ya kwenda Ujiji na Kasulu. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021** siku ya Jumatatu saa 1:30 asubuhi. Kwa hiyo, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** (ndani ya siku saba)

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

**A. WAVULANA**

i. Suruali 2 nyeusi za kitambaa aina ya "**Istem**" ziwe na linda za mbele, isibane na iwe na mifuko mitatu. Upana wa chini usipungue **nchi 16** na iwe na **Turn by**. Tafadhali sana zingatia hatutaki modo kinyume chake utaondolewa shule.
ii. Shati 2 nyeupe zenye mikono mifupi na zisiwe na marembo yoyote.
iii. Vizibao vyeusi 2 aina ya kitambaa cha suruali pamoja na Tai nyeusi ndefu 2.
iv. Mkanda wa ngozi mweusi wenye chuma kidogo kisicho na marembo yoyote.
v. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba visivyo na visigino virefu Jozi mbili pamoja na soksi nyeusi jozi mbili.

**B. WASICHANA**

i. Sketi 2 nyeusi za kitambaa aina ya "**Istem**" zenye mshono wa **Linda box ya mbele** na ziishie kwenye kifundo cha mguu wala zisibane mwili. Tafadhali sana zingatia hatutaki vimini kinyume chake utaondolewa shule.
ii. Shati 2 nyeupe zenye mikono mifupi na zisiwe na marembo yoyote.
iii. Vizibao vyeusi 2 aina ya kitambaa cha sketi pamoja na Tai nyeusi ndefu 2.
iv. Wanaopenda kuvaa hijabu, wanatakiwa kushona hijabu ndefu inayofunika mikono, kitambaa cha Tetron nzito isiyoonesha kiwe na rangi nyeupe. (*Mwenye hijabu asishone kizibao*).
v. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba visivyo na visigino virefu Jozi mbili (02) pamoja na soksi nyeupe jozi mbili.

**ANGALIZO KWA WOTE:**

- Sare iliyokosewa mshono haitakubaliwa shuleni
- Mwanafunzi anatakiwa muda wote kuwa amechomekea shati lake na kufunga tai na kizibao kiwe kimefungwa.
- Atakayependa kuvaa **Sweta,** wakati wa baridi tu, liwe la **rangi ya Kijivu**.

**C. SARE ZA MICHEZO**

Sare ya michezo kwa **Wavulana** ni fulana ya rangi ya kijani nzito isiyo na maandishi / picha yoyote, bukta ya bluu na raba. **Wasichana** hivyo hivyo ila wao wanaongeza Sketi Nyekundu yenye michirizi miwili ya kijani pembeni upande wa kulia.

**2.2 VIFAA VYA TAALUMA**

i. Daftari kubwa **Size 12A** au **Kaunta Book 2Q** zisizopungua 11.
ii. Kalamu za bluu au nyeusi za kutosha, penseli, rula na kifutio.
iii. Mkebe wa hesabu (Mathematical Set 1)
iv. Msaidie mwanao katika kupata vitabu vya kumsaidia kujiimarisha katika lugha ya Kiingereza kama vile Mabala the Farmer, Hawa the Bus driver,n.k

**2.3 MAHITAJI MENGINEYO**

Shule yetu ni ya kutwa hivyo chakula cha Wanafunzi, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu ni jukumu la mzazi. Shule itahusika na huduma ya kwanza na kuwasiliana na mzazi.

**3.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

A. "Medical Examination Form" ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

B. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

C. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. (Mzazi asome mwenyewe maelezo ya fomu hiyo au asomewe kwa wale wasiojua kusoma na kuandika na aweke sahihi yake au alama ya dole gumba, kisha apewe nakala yake.

D. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

**4.0 TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO / MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.**

**KARIBU SANA MWANANCHI SEKONDARI**

Wabera
...............

MKUU WA SHULE
MWANANCHI SEKONDARI
S.L.P. 53
KIGOMA

**MAXIMINUS M. WABERA**

**MKUU WA SHULE.**

**NAMBA YA SIMU : 0754 974118.**

## OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA

## SHULE YA SEKONDARI MWANANCHI

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978** na kama ilivyorekebishwa kwa **Sheria Na. 10 ya mwaka 1995**. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi wa Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni ( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule kwa usahihi wakati wote unapotakiwa,tafadhali sana zingatia kwa kina.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
ix. Kutunza mali za umma.

## MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

i. Wizi.
ii. Uasherati na ushoga.
iii. Ubakaji.
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile ujutaji bangi cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
v. Kupigana au kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii. Kudharau Bendera ya Taifa.
viii. Kukataa / kugomea adhabu kwa makusudi.
ix. Kuwa mjamzito / kupata mimba.
x. Kuoa au Kuolewa.
xi. Kutoa mimba.
xii. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
xiii. Kuwa na simu ya mkononi.
xiv. Utoro wa siku tisini (90) mfululizo au kutoroka Mitihani.

FORM A

## HISTORIA YA MWANAFUNZI NA UKOO WAKE

1. Jina kamili la Mwanafunzi: ..........................................................................................
2. Dini / Dhehebu: .................................... Tarehe ya kuzaliwa: ..................................
3. Jina kamili la baba mzazi / Ndugu / Mlezi anayeishi nae ..............................................

   Anuani: Kijiji / Mtaa / ..........................................................................................

   S. L. P .................................................. SIMU: ....................................

   Kazi yake ..........................................................................................

   Mahali anapofanyia kazi ..........................................................................
4. Jina kamili la mama mzazi / Ndugu / Mlezi anayeishi nae ..............................................

   Anuani: Kijiji / Mtaa / ..........................................................................................

   S. L. P .................................................. SIMU: ....................................

   Kazi yake ..........................................................................................

   Mahali anapofanyia kazi ..........................................................................
5. Habari za jamaa na familia (Ukoo) wanaoweza kukusaidia wakati wa matatizo

| Na | JINA KAMILI | UMRI | UHUSIANO | KAZI YAKE | ANUANI | SIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |
| 5. | | | | | | |
| 6. | | | | | | |
| 7. | | | | | | |
| 8. | | | | | | |
| 9. | | | | | | |
| 10 | | | | | | |

### JIOGRAFIA YA MAKAZI

1. Jina la Mtaa unaoishi ................................................ Namba ya nyumba .................
2. Jina la Kata ..........................................................................................

### KIAPO CHA KUFUATA SHERIA ZA SHULE NA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO

Mimi ................................................................................ ninakiri kwamba nitafuata sheria zote za shule na kwamba kwa kipindi chote nikiwa Mwanafunzi wa shule hii sitoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Na pia nitahudhuria shule bila kukosa ikiwa ni pamoja na kuwahi siku ya kwanza ya kufungua shule.

**Sahihi ya Mwanafunzi** ................................................ **Tarehe**: ..................................

FORM B

## SHULE YA SEKONDARI MWANANCHI

## MKATABA WA MZAZI / MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.

**Mimi** ............................................................................ **Umri**: .................. Ninayeishi mtaa wa ........................................... **Kata**: ............................. Katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma / Ujiji. Ambaye katika Mkataba huu ninatambuliwa kama **Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi** ........................................................................ **wa kidato cha** ............ **Mwaka**: .............

Nathibitisha kwamba:

1. Nimesoma na kuzielewa vizuri sheria na kanuni za shule hii kama zilivyoambatanishwa katika fomu ya maelekezo muhimu ya mwanafunzi kujiunga na shule hii, na kwamba * **Nakubaliana / Sikubaliani** nazo.
2. Nitahakikisha mwanangu anafika shuleni kila siku ya kwanza ya shule kufunguliwa na ikitokea dharura nitatoa taarifa ya maandishi shuleni wiki moja kabla ya shule kufunguliwa na kwa vyovyote vile Mwanafunzi atapaswa kuripoti shuleni si zaidi ya wiki moja tangu shule kufunguliwa.
3. Nitahakikisha mwanangu anahudhuria shuleni siku zote za masomo, anaandika na kufanya mazoezi yote ya darasani na mitihani bila kukosa katika kipindi chote akiwa Mwanafunzi.
4. Nitafuatilia kwa ukaribu maendeleo ya mwanangu kitaaluma na kushirikiana na walimu vizuri katika kuinua taaluma yake.
5. Ikitokea mwanangu amevunja sheria, kanuni na taratibu za shule hatua stahiki zichukuliwe dhidi yake na nitashirikiana na uongozi wa shule katika kuhakikisha mwanangu anakua na tabia njema na mwenendo mzuri kwa kipindi chote akiwa mwanafunzi.
6. Nitahudhuria vikao vyote halali vya wazazi vitakavyoitishwa shuleni ili kujadiliana namna bora ya kuboresha elimu na nitafika shuleni kuchukua matokeo / nitahakikisha mwanangu ananiletea matokeo ya mitihani yote itakayokuwa ikifanyika shuleni.
7. Nitafuata njia sahihi kuomba ruhusa ya Mwanafunzi na kutoa taarifa mapema shuleni ikitokea mwanangu ni mgonjwa. Njia sahihi ni kufika shuleni kutoa taarifa kwa mwalimu wa zamu / darasa; au kwa Makamu Mkuu wa Shule kwa ruhusa ya muda mrefu (zaidi ya wiki moja).

* **Nakubaliana / Sikubaliani** na vipengele vyote vya mkataba huu na kwamba itahesabika ni kosa kisheria Mwanafunzi akishindwa kufika shuleni na kuhudhuria masomo kutokana na uzembe wangu. Ikitokea hivyo, sheria ichukue mkondo wake mara moja dhidi yangu.

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe ................................................... kati yangu

**Jina:** ............................................................................. **Sahihi:** ....................................... (Mzazi wa Mwanafunzi)

**Mbele ya: Jina:** ............................................................. **Sahihi:** ................................ **Tarehe:**...................

**Muhuri wa Ofisi:** .............................................................................

(Shahidi lazima awe Mwenyekiti wa Mtaa / Mtendaji)

**Futa isiyo husika.*

FORM C

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING
## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

*To be completed by a medical Officer in respect of all Form One entrants.*

*Pupil's Full Name:* ..............................................................................................

*Age:* .......................... *Year of Birth:* ........................................ *Sex:* ..................

*Blood found (Red and White)* ....................................................................

*Stool Examinations:* ..............................................................................

*Urinalysis:* ........................................................................................

*Syphilis and Other:* ..............................................................................

*Venerable Diseases Test:* ......................................................................

*T. B Test:* ...........................................................................................

*Eye Test:* ...........................................................................................

*Ears:* ...............................................................................................

*Chest:* ..............................................................................................

*Spleen:* ............................................................................................

*Abdomen:* .........................................................................................

*Urine Test for Pregnancy:* ......................................................................

*Additional information (If any e.g. Physical defects impairment(s)*

*( e.g. arm, leg, etc ) infection chronic or families diseases etc.*

.........................................................................................................

.........................................................................................................

.........................................................................................................

.........................................................................................................

*I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.*

Signature: ..............................................

Destination: ..........................................

Station: ..............................................

Date: ..............................................